

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR**

08/05/2024

**TAARIFA KWA UMMA JUU YA BEI ZA MAFUTA KWA MWEZI MEI 2024.**

Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inatangaza Bei za Mafuta kwa Mwezi Mei 2024 zitakazoanza kutumika rasmi kuanzia Siku ya Alkhamis, Tarehe 09/05/2024.

Mamlaka hupanga bei kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za Mafuta Duniani (Platts Quatations).
- Gharama za uingizaji Mafuta katika bandari ya Dar-es-Salaam na Tanga.
- Gharama za Mabadiliko ya Fedha za kigeni zinazotumika kununulia mafuta.
- Gharama za Usafiri, Bima na 'Premium' hadi Zanzibar.
- Kodi na Tozo za Serikali.
- Kiwango cha faida kwa Wauzaji wa Jumla na Reja Reja.

Bei za mafuta kwa Mwezi Mei, 2024 ni kama zifuatazo:

AINA YA MAFUTA	BEI YA MWEZI APRILI, 2024 (TZS/LITA)	BEI YA MWEZI MEI, 2024 (TZS/LITA)	TOFAUTI (TZS/LITA)	TOFAUTI ASILIMIA
PETROLI	3,133	3,182	49	1.56
DIZELI	3,165	3,146	-19	-0.60
MAFUTA TAA	3,200	3,200	0	0
MAFUTA NDEGE	2,792	2,790	-2	-0.07

Sababu za kuongezeka kwa Bei ya Petroli ni kuongezeka kwa gharama za Mafuta katika Soko la Dunia, na sababu za kupungua kwa Bei ya Dizeli na Mafuta ya Ndege ni kupungua kwa gharama za Mafuta katika Soko la Dunia na kupungua kwa gharama za uingizaji wa mafuta pamoja na mabadiliko ya Fedha za kigeni.

Mamlaka inawahimiza Wananchi kununua Mafuta katika Vituo halali vya Mafuta na kudai Risiti za Kielektroniki kila wanaponunua Mafuta.

**IMETOLEWA NA KITENGO CHA UHUSIANO (ZURA)**



+255 24 294 1190  
S.L.P 2238



info@zura.go.tz  
zura.go.tz



Makao Makuu ZURA  
25 Barabara ya Julius Nyerere  
70473 Mjini Magharibi, Maisara, Zanzibar